# THE SKY'S LIMIT AFRICA:

*The case for a just energy transition from fossil fuel production in Africa*

# Muhtasari

Mwezi wa Mai 2021, shirika la Kimataifa la Nishati (IEA) kilitoa taarifa yake ya kimataifa ya kwanza ya mfano uliotangamanifu na kupunguza ongezeko la joto duniani kwa nyuzi joto 1.5 (°C). Shirika hilo lilipata kuwa mabomba mapya ya mafuta, gesi na nishati za asili na migodi ya makaa ya mawe si tangamanifu na lengo kuu la tabia nchi. Ripoti hiyo ya IEA ilichochea kuwa utafiti uliofanywa na shirika la kimataifa la Oil Change na nyinginezo zinaonyesha kuwa kuna haja ya kuondolewa kwa viwanda vya nishati za kiasili kwa dharura ili kueupekana na athari kali za mabadiliko ya tabia nchi.

Athari za mabadiliko ya tabianchi, gharama ya kibinadamu, na hatari za kiuchumi zinazoletwa na mafuta, gesi na miradi ya makaa ya mawe inamaanisha kuwa miradi mipya ya kupekecha mafuta ya nishati za asili isiidhinishwe – Afrika ama kokote. Ripoti hii inadai kwamba kuondolewa kwa viwanda vya kutengeneza nishati za kiasili Afrika kwa utaratibu na usawa pamoja na mabadiliko ya kutumia nishati mbadala na uchumi wa kidemokrasia unaozingatia mazingira. Kuondolewa kwa viwanda vya kutengeneza nishati za kiasili si lazima kusimamishe ghafla matumizi na utengenezaji wake barani Afrika. Ilhali, inamaanisha kuanza kupanga kwa upana sasa ili kuhakikisha kuna muda na rasilimali za usafishaji na pia mabadiliko ya haki kwa wafanyikazi na wanajamii wanaotegemea utengezaji wa nishati za asili.

Gharama ya kuondelewa kwa nishati za asili haiwezi kuwa jukumu la kipekee kwa usawa**. Nchi zilizotajiri Ulimwenguni Kaskazini zinazodaiwa kihistoria na kisasa kutoa gesi zilizo na athari kali lazima ziwe za kwanza kuondoa utengenezaji wa nishati, tena kwa kasi; kisha walipie haki yao katika mabadiliko ya kimataifa ya nishati mbadala.**

Mikataba isiyofaa, ruzuku za viwanda vinavyofaa na mifumo ya hakimiliki, madeni, ufisadi na mashirika ya kimataifa ambayo yanaumiliki mkubwa wa rasilimali ya nishati za asili, vyote vinamaanisha kuwa utengenezaji wa nishati za asili Afrika havijasaidia kihistoria kama chombo cha maendeleo, upatikanaji wa nishati, au rasilimali za enzi kuu. Uwezekano wa sekta hii


kudumisha maendeleo umedidimia kwa sababu ya ongezeko la hatari za kiuchumi. Serikali zinazochagua kufuatilia uvumbuzi mpya wa kupekecha mafuta, gesi na makaa ya mawe sasa wanajiweka hatarini kwa kujifungia nje ya mabadiliko kuelekea katika nishati mbadala na sekta nyingine zinazozingatia mazingira.

## Kupekecha nishati za asili ≠ maendeleo, ajira, au upatikanaji wa nishati

Tunaanza na kuangalia athari za utengenezaji wa nishati za asili Afrika mpaka sasa, na kuchunguza jinsi ongezeko la athari hizi zinahusikaje na matokeo haya katika sekta hii.

- **Kuwacha watu wengine nyuma ilhali kutuza mashirika ya kimataifa na kufungia nishati mbadala:** Faida nyingi zinazotokana na mpekecho zinatiririka ng'ambo badala ya barani Afrika. Mchoro 1 unaonyesha 60% ya makadirio ya utengenezaji katika miongo mitatu ijayo itasababishwa na mashirika ya kimataifa. Hali hii inaweza kuzoroteka: tunapozingatia miradi mipya ya utengenezaji, 66% inamilikiwa na mashirika ya kimataifa, zikiongozwa na Total, Eni, ExxonMobil, na BP.

**Mchoro 1: Nani anafaidika? Makadirio ya Utengenezaji wa Mafuta na Gesi katika Bara la Afrika, % Umiliki wa Maeneo, 2020 – 2050.**




*Kwa hisani: Taarifa ya uchambuzi wa Shirika la Oil Change kutoka kwa Rystad UCube. Kutoka kwa makao makuu ya kampuni.*

- **Kukosa kutimiza ahadi za faida ya ajira na upatikanaji wa nishati unaotokana na maendeleo.**

Katika bara la Afrika, sekta za upekechaji zinaajiri chini ya asilimia moja ya watendakazi wa Afrika; wakaazi wa eneo hili wamepata kazi chache zinazolipa vizuri na za kudumu. Ukilinganisha na uwekezaji wa dola moja, nishati mbadala zimeunda ajira zaidi mara 2.5 hadi 5 kushinda nishati za asili, na vitega uchumi vinavyozingatia mazingira kama ukulima unaozingatia uhifadhi, kukabiliana na tabianchi, usafiri wa umma na majengo yatakayohifadhi nishati zinafanisi na kutoa ajira zaidi mara 5 hadi 25. Afrika huuza nje mafuta, gesi na makaa ya mawe. Miundombinu ya sasa na iliyopangiwa imebuniwa kusambazwa kwa uchumi wa ng'ambo badala ya kuzingatia upungufu wa nishati barani Afrika.

- **Kuhatarisha afya, ajira na mazingira ya wanajamii.**

  Wanajamii wanaoishi karibu na sehemu za upekechaji wamekabiliwa na kuhama, kupoteza kazi kwa sababu ya uharibifu wa mashamba, uvuvi au utalii, shida kali za kiafya, kuzoroteka kwa mazingira, kudhulumiwa kwa haki za binadamu, na kuongezeka kwa vita na matumizi ya nguvu za kijeshi.

- **Uungamanishaji wa udhaifu wa tabianchi Afrika.** Afrika imechangia asilimia mbili pekee ya gesi za viwanda tangu 1890 mpaka sasa. Hata hivyo, kulingana na mabara mengine, Afrika imeathirika zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na ina wasilimali chache zaidi ya kukabiliana na athari hizi.

- **Kuweka mali ghafi za kuuza nje zilizo na athari ilhali kuzuia nishati mbadala na sekta nyinginezo zinazohifadhi mazingira**. Afrika ina uwezo wa kutoa asilimia 39 ya nishati mbadala duniani. Kudumisha maendeleo ya nishati za asili ilhali sekta hii inakumbwa na changamoto zisizo na kifani itatatiza uwezo usiolinganika wa Afrika kuzindua nishati inayotokana na jua na upepo.

## Mipango ya sekta ya nishati za asili inaathari kubwa kwa uchumi na tabianchi barani Afrika

Yanayofuata, tunaonyesha makadirio ya jumla ya taswira ya utengenezaji wa nishati mbadala na pia utengenezaji unaotokana na miradi mpya Afrika mnamo Mwaka wa 2020 na 2050, kutumia kielelezo kutoka kwa kampuni ya mashauriano ya Rystad Energy. Tunabainisha kuwa:

- **Utengenezaji wa nishati ya asili ukitoa mafuta, gesi na makaa ya mawe barani Afrika miongo mitatu ifuatayo, itatoa tani bilioni 65 za $CO_2$.** Kiwango hiki ni sawa na asilimia 13 ya bajeti ya kaboni inayohusika na asilimia 50 ya kudumisha kiwango cha joto duniani chini ya nyuzi joto 1.5(°C).

- **Utengenezaji wa nishati mbadala Afrika ulipunguka zaidi ukilinganisha na maeneo mengine kwa sababu ya mitikiso mwaka wa 2020, na kiwango kikubwa kihatarini ni bidhaa zilizoharibiwa, kuendelea mbele.** Badala ya kuongezeka hadi asilimia 32 mnamo mwaka wa 2050 kama ilivyotajiriwa kabla ya 2020, utengenezaji wa mafuta na gesi Afrika unatarajiwa kupungua kwa asilimia 24. Awali kiwango hiki kilikuwa thabiti hadi 2050, lakini upekechaji wa makaa ya mawe unatarajiwa kupungua kwa asilimia 14. Asilimia sitini na nane ya utengenezaji wa mafuta na gesi itakayokuzwa na miradi

isiyoanza bado mnamo mwaka wa 2020 hadi 2050 inasemekana kutokana na upekechaji wa maji ya kina kirefu au upekechaji mzito ambao unaathiri zaidi siku za mbele.


- **Asilimia thelathini na moja ya utengenezaji upo katika nchi saba "mpya" zilizo hazina upekechaji au zinaupekechaji kiasi wa mafuta na gesi.** Nchi saba zinazotarajiwa kuwa mojawapo ya 16 zitakazoongoza katika upekechaji wa mafuta na gesi katika bara la Afrika kutoka sasa hadi 2050 ni mpya katika sekta hii (Msumbiji, Tanzania, Mauritania, Afrika Kusini, Senegali, Uganda na Uhabeshi). Miradi iliyopangwa katika nchi hizi itakuwa na gharama zaidi inayotokana na ujenzi wa muundombinu na mifumo ya udhibiti inayohusika na upekechaji.

- **Asilimia arobaini ya gesi zinazotokana na upekechaji wa nishati za asili Afrika bado haujatolewa.** Kuanzia 2020 hadi 2050, asilimia 46 ya utengenezaji wa gesi, asilimia 36 ya uzalishaji wa mafuta, na asilimia 23 ya makadirio ya uzalishaji wa makaa ya mawe inakadiriwa kutoka kwa miradi mipya ambayo haiko katika utengenezaji au chini ya maendeleo kwa sasa.

- **Mipango ya viwanda vya utengenezaji wa nishati inaweza kuunda hadi $ 230 bilioni ya mali iliyokwama kutoka kwa mafuta na uzalishaji mpya barani Afrika katika mwongo mmoja ujao, na trilioni $ 1.4 ifikapo mwaka 2050.** Hizi ndizo pesa ambazo sekta ya mafuta inatarajia kuwekeza katika uvumbuzi na maendeleo ya miradi mpya ya mafuta na gesi ambayo haijakubaliwa katika miaka 10 na 30 ijayo. Ikiwa utenguaji na upokeaji wa haraka wa nishati mbadala utaendelea, uwekezaji huu mwingi unaweza "kukwama," na kuunda mahitaji - lakini sio fedha - za kusafisha uharibifu wa mazingira, upotezaji wa kazi mara moja, na upungufu wa mapato ya serikali.


- **Sehemu ya sekta hiyo inaendelezwa na fedha za umma kutoka kwa serikali tajiri na zinazochafua, ambazo zinatarajiwa kufifia.** Kati ya 2016 na 2019, nchi za G20 zilitoa $47 bilioni kwa fedha za umma kwa nishati za asili barani Afrika, mara 3.7 kiwango kilichotolewa kwa nishati mbadala. Walakini, hali hizi zinaanza kubadilika. Wakati uchumi wa EU, Uingereza, na Marekani kati ya uchumi mwingine mkubwa unapoamua kuondoa fedha hizi za kimataifa za umma, matarajio ya kiuchumi ya mafuta, gesi, na makaa ya mawe barani Afrika yanatarajiwa kurudi nyuma zaidi ya sekta zingine - pamoja na ushindani wa kifedha wa nishati mbadala uliopo tayari.

**MCHORO 2: Makadirio ya gesi zinazotokana na utengenezaji wa mafuta, gesi na makaa ya mawe katika nchi zote za Afrika, kulingana na kiwango cha akiba, mwaka wa 2020 – 2050, tani bilioni za $CO_2$**




*Kwa hisani: Taarifa ya uchambuzi wa Shirika la Oil Change kutoka kwa Rystad UCube.*

**MCHORO 3: Nchi 16 Afrika zinazoongoza katika utengenezaji wa mafuta na gesi kutoka kwa miradi mipya isiyoidhinishwa (2020 - 2050)**




*Kwa hisani: Taarifa ya uchambuzi wa Shirika la Oil Change kutoka kwa Rystad UCube*

Katika ripoti hii, pia tunaangazia athari zingine za ukuzaji wa mafuta katika nchi maalum na harakati za nguvu za watu zinazopigania kuzizuia:

- Harakati za mabadiliko yaliyo na haki kutoka makaa ya mawe nchini **Afrika Kusini**
- Mapambano dhidi ya Bomba la Mafuta Ghafi la **Uganda-Tanzania** la Afrika Mashariki (EACOP) ambalo nihatari kwa uchumi na mazingira

- Vifungu vya kuchukua-au -kulipa katika kandarasi ya mafuta na gesi ambayo imesababisha deni kurundikana na kuziba nishati mbadala nchini **Ghana**
- Upinzani wa ukiukaji wa haki za binadamu pamoja na ukandamizaji mbaya wa mashirika ya kijamii na vile vile athari za mazingira na afya za wenyeji nchini **Nigeria**
- Kashfa ya **Senegal** ya Petro-Tim, mfano wa kodi ya rasilimali inayoishia kwenye mifuko ya kibinafsi na akaunti za kigeni badala ya hazina ya umma na miradi ya nchini humo
- Mipango ya Total ya maendeleo makubwa ya LNG barani Afrika iliyoko **Msumbiji**. Maendeleo haya ya LNG yakichanganyika na utofauti wa utajiri unaokua, athari za tabianchi, na uharibifu wa mazingira wa karibu ili kuchochea mizozo.

## Mapendekezo

Mwaka 2020 ulitoa muhtasari wa jinsi kutokomea kusikodhibitiwa kunaweza kuonekana katika sekta ya mafuta na gesi ulimwenguni. Mchakato huu umeathiri nchi na jamii zilizo katika mazingira magumu zaidi, pamoja na nyinginezo zinazotegemea zaidi usafirishaji wa mafuta na gesi nje ya barani Afrika. Haki ya mazingira na harakati zingine za kijamii barani Afrika zimekuwa zikipambana kwa muda mrefu, **kujitenganisha na nishati za asili kunatoa fursa ya kujenga mfumo wa nishati na uchumi mpana ambao ni wa ndani, ulio na usawa, na kidemokrasia.**

Hali ya kuwa na mabadiliko kwa njia ya haki itahitaji maamuzi ya ndani na mashauriano ili kuruhusu jamii kuamua jinsi mabadiliko ya nishati yanapaswa kuonekana katika maeneo yao. Walakini, tunaweka kanuni kadhaa pana za jinsi jamii zetu zinaweza kubadilishwa kuwa na uchumi unaozingatia urejeshi, haki, na kuzaliwa upya lazima ujumuishe: kuepukana na nishati za asili, harakati kali za kijamii na vyama vya wafanyikazi, mipango ya haki ya kuepukana na nishati za asili, ikiongozwa na kupangwa na wafanyikazi katika kampuni za nishati za asili na jamii zilizoathiriwa, tofauti za kiuchumi na zinazozingatia watu na dunia akilini, nishati mbadala kwa wote, kukuza umiliki wa wananchi na udhibiti wa rasilimali kidemokrasia, uhuru wa chakula, kukataa suluhisho bandia na harakati za upekechaji, kukuza ushirikiano wa kina katika maeneo, na kuhakikisha wachafuzi wa mazingira wanalipia uharibifu ambao wamesababisha.

Kuunda Ujumbe wa Mkutano wa Viongozi wa Nishati wa Afrika 2020 na mfumo wa awamu ya usawa ulimwenguni kuwacha matumizi ya nishati za asili kwa hisani ya Muttitt na Kartha (2020),[1] tunatoa mapendekezo ya msingi yafuatayo kwa serikali za Afrika:

- **Ambapo utengenezaji wa nishati za asili tayari umeanzishwa:**
    - Tengeneza mipango ya kusimamia kumaliza miradi iliyopo ya kutengeneza nishati za asili hatua kwa hatua kabla ya 2050, pamoja na mabadiliko ya haki kwa wafanyikazi na jamii.

[1] Greg Muttitt and Sivan Kartha, "Usawa, haki ya tabianchi na uchimbaji wa mafuta: kanuni za awamu inayodhibitiwa," *Sera ya tabianchi*, 20:8 (2020): k. 1024
-1042, http://www.tandfonline.com/10.1080/14693062.2020.1763900.

    - Weka kipaumbele kumaliza miradi ambayo inahatarisha zaidi haki za binadamu, na ambayo jamii zilizotengwa zimepata athari mbaya zaidi za utengenezaji wa nishati za asili.
    - Tekeleza sera za viwandani na kijamii kuelekeakuwa na  mseto wa uchumi, kuweka msisitizo kwa sekta za kaboni ndogo ambazo pia zinaunda jamii zilizoimara na za usawa na mipango iliyoshirikishi.

- **Katika nchi zote, pamoja na ambazo utengenezaji wa nishati za asili umepangwa lakini haujaanzishwa tayari:**
    - Ongeza kwa kasi usanikishaji wa nishati mbadala - haswa nishati mbadala inayosambazwa katika maeneo ya gridi ya taifa - kufikia upatikanaji wa nishati kwa wote.
    - Kataza kutoa leseni na idhini ya miradi mipya ya nishati za asili.
    - Fuatilia maendeleo ya haraka ya rasilimali zisizo na kifani za nishati ya jua na upepo barani Afrika kutekeleza ufikiaji wa nishati kwa wote kabla ya mwaka wa 2030 na kujiunga zaidi na mifumo ya nishati mbadala na inayosambazwa.

Katika ripoti hii, tunasisitiza kwamba serikali za nchi tajiri lazima pia zishiriki kwa usawa na haki. Tunatoa mapendekezo ambayo yatahakikisha (a) wanabadilisha kwanza na kwa haraka katika kumaliza utengenezaji wa nishati za asili, (b) kusitisha fedha za nishati za asili na vitendo vingine vinavyozuia mabadiliko ya haki ya nchi za Afrika, na (c) kulipia kuunga mkono mabadiliko ya haki kutoka kwa nishati za asili Afrika nzima, na katika nchi zote za Ulimwenguni Kusini kulingana na jukumu lao la kihistoria na linaloendelea linalohusiana na matatizo ya mabadiliko ya tabianchi.